**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI DAR ES SALAAM GIRLS**

**S.L.P 55068 DAR ES SALAAM, Email: daressalaamgirlssec@gmail.com,SIMU:0655748374(MKUU WA SHULE)**

Mzazi/Mlezi wa ……………………………………

S.L.P ………………………………………………….

…………………………………………………………

**KUH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA (I) MWAKA 2026**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa binti yako amechaguliwa kujiunga katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya **DAR ES SALAAM GIRLS**. Shule hii ni ya bweni na Kaulimbiu ya shule yetu ni "***The home of Scientists"*** hivyo mwanafunzi awapo shuleni hapa anatakiwa aendane na kaulimbiu yetu kwa kusoma kwa bidii.

Wanafunzi wanatakiwa kuripoti shuleni siku ya**… /01/2026** kuanzia saa **nne (4:00) kamili** asubuhi mpaka saa **kumi (10:00) kamili jioni**. Masomo yataanza rasmi siku ya tarehe…… **/01/2025.**

## MUHIMU SANA

Wanafunzi watakaofika baada ya siku 14 tangu shule kufunguliwa bila sababu za msingi hawatapokelewa. Binti yako atatakiwa kukamilisha taratibu zote kabla ya kusajiliwa shuleni

## 2.0 JINSI YA KUFIKA SHULENI

Shule ipo Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, Mtaa wa Njeteni, Kata ya Kwembe, kilometa 2.4 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Ubungo (Luguruni).

### 2.1 Kwa kutumia Usafiri wa Umma

Ukitokea Mbezi, panda daladala inayoelekea Kibamba /Mloganzila au Mlandizi, shuka kituo cha Chuo Kikuu cha St. Joseph mkabala na kituo cha Mafuta cha Henry. Kisha panda pikipiki (Tsh 1,000) itakayokufikisha shuleni.

### 2.2 Kwa wenye Usafiri Binafsi

Ukitokea Mbezi kuelekea Kibamba, fika round about ya Mbezi kwa Yusuf, kisha fuata njia ya vumbi mpaka hotel ya Wilivina utakuta Kibao cha Barabara ya Njeteni, fuata uelekeo wa Barabara hiyo, itakufikisha shuleni.

### 2.3 Ukitokea Kibaha au Kibamba

Fika eneo la Luguruni na fuata barabara inayoelekea kwa Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, elekea mbele utakuta Kibao cha barabara ya Njeteni, fuata uelekeo wa barabara hiyo itakufikisha shuleni.

**KARIBU SANA**

## 3.0: SARE ZA SHULE

### *3.1: Sare ya Darasani*

- Sketi mbili za kitambaa cha aina ya "Mallard Green" zenye urefu wa kufika kwenye vifundo vya miguu;
- Mashati meupe (tomato) mawili au zaidi ya mikono mifupi;
- Soksi ndefu (free size) nyeupe jozi nne au zaidi;
- Sweta moja la rangi ya kijivu;
- Tshirt 1 ya rangi ya zambarau yenye Kola (Form six); na
- Viatu vya rangi nyeusi vya kudumbukiza vya kike vyenye uwazi juu (Juma na



  Roza). Viatu vya plastic au viatu vya aina nyingine havitaruhusiwa darasani (**Kwa mzazi atakayependa sare zote zinapatikana kwenye duka lililopo Jirani na shule isipokuwa viatu)**

***NYONGEZA***

Kwa wanaovaa hijabu watashona nusu kanzu nyeupe (badala ya shati) yenye urefu wa kufunika mikono na ifike chini ya makalio. Aidha Ushungi (juba) uwe mweupe wenye kufunika mikono usio na urembo wowote.

### 3.2: *Sare ya Kushindia*

- Gauni ya solo yenye rangi ya **LIGHT BLUE** ambalo ni lefu hadi kwenye vifundo vya miguu, shingo ya duara na mikono mifupi.

### 3.3: *Sare wakati wa kujisomea jioni (Evening preparation)*

- Trucksuit ya rangi ya light blue; na
- T-shirt moja (1) ya **KOLA** ya rangi ya light.

### 3.4: *Sare ya Michezo*

- Trucksuit ya rangi ya kijivu (gray);
- Jezi ya na bukta ya rangi ya njano;
- Raba nyeupe jozi moja.

***(Kwa mzazi atakayependa sare zote zinapatikana kwenye duka lililopo jirani na shule isipokuwa viatu)***

## 4.0: MAHITAJI MENGINE

### 4.1: *Vifaa vya Kitaaluma*

- Madaftari makubwa kumi na moja (11) (Counter books quire 3);
- Madaftari 11 aina ya `msomi kwa ajili ya mazoezi;
- Rimu mbili (2) nyeupe kwa muhula mmoja za aina ya **A-ONE AU PAPER LINE;**
- Begi la rangi nyeusi la kubebea madaftari;
- Spring file moja kwa ajili ya kuwekea nyaraka zake awapo shuleni; na
- Vitabu vya ibada kwa mujibu wa dhehebu/dini yake;
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa **NI LAZIMA AJE NAYO**;
- "Mathematical Set", Kalamu za Wino, Risasi, Rula, Kamusi (02), moja ya Kingereza kwa Kiswahili (English- Kiswahili) na moja ya Kingereza (English-English);
- Picha tatu (Passport size) akiwa amevaa shati la shule na ya mzazi au mlezi; na
- Kwa kuwa shule ina nakala chache za vitabu kwa ajili ya masomo utakayochukua, **inashauriwa** kama unaweza kupata vya kwako binafsi (Vitabu vya Kiada na Rejea) uje navyo.

### *4.2: Vifaa vya Usafi*

(i) Soft broom (fagio laini) moja (01);
(ii) Jembe moja (01);
(iii) Fagio ngumu (hard broom) moja (01);
(iv) Ndoo ndogo mbili (02);
(v) Squizzer moja (01);
(vi) Mopa kubwa na ndoo yake moja (01);
(vii) Brashi ndogo ya chooni Moja (01);
(viii) Fyekeo lililonolewa moja (01)

**4.3:** ***Mahitaji ya Bwenini***

(i) Godoro futi **3** kwa **6** (**Jipya**), vitanda vyetu ni vikubwa hivyo godoro liwe futi **3** upana, urefu futi 6 na unene inchi **sita** (**Mzazi atakayependa godoro linapatikana kwenye duka lililopo jirani na shule kwa bei ya jumla);**

(ii) Shuka mbili (02) za rangi ya pink pamoja na mto na foronya (rangi ya pink);

(iii) Chandarua nyeupe ya pembe nne, futi nne kwa sita (6x4) na blanket kwa wenye changamoto ya kiafya;

(iv) Tochi au taa ya solar kwa tahadhari ya umeme ukikatika;

(v) Taulo moja (01), jozi moja vitenge au khanga (nguo zisizotajwa haziruhusiwi;

(vi) Vyombo vya chakula, sahani, bakuli, kikombe na kijiko (vyote viwe vya mfupa);

(vii) Chupa ya maji ya kunywa na galoni la lita tano la kuhifadhia maji ya kunywa;

(viii) Sabuni za kuogea na kufulia za kutosha, mswaki na dawa ya meno, mafuta ya kupaka na ya nywele na losheni yasiyo na harufu kali, deodorant (parfume na spray haziruhusiwi), taulo za kike, taiti na sidiria iwe nyeupe au nyeusi, chupi zisizopungua 6;

(ix) Sanduku la chuma kubwa lenye kufuri mbili;

(x) Ndoo kubwa moja na ndogo moja zenye mifuniko kwa ajili ya usafi wake binafsi;

(xi) Jozi moja (01) ya kandambili (mpya) na pea moja ya viatu vya wazi pamoja na yeboyebo;

(xii) Nguo mbili za kulalia usiku (night dress) za rangi ya blue;

(xiii) Pesa za matumizi madogo madogo zisizozidi Tsh: 50,000/= ( kwa usalama zitatunzwa na Matron)

**ANGALIZO**

(i) Wanafunzi hawaruhusiwi kuleta vyakula vya aina yoyote shuleni, nguo za nyumbani, vitu vya thamani kama kamera, radio, simu za mkononi, head & earphone, na vitu vinavyoweza kusababisha ajali ya moto kama mishumaa, viberiti, taa za kandili n.k;

(ii) Mzazi utakapofika shuleni utakabidhiwa barua ya makubaliano ya wazazi inayoelezea mipango na mikakati ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kuinua ufaulu na miundo mbinu ya shule;

(iii) Shule haitoi chakula maalum cha mgonjwa (special diet), pia mwanafunzi haruhusiwi kuwa na chakula cha aina yoyote bwenini;

(iv) Wanafunzi wenye **BIMA YA AFYA** waje nazo. Kwa wale ambao hawana lazima waje na shilingi elfu hamsini na nne (Tsh. 54,000/=) ambapo (50400 ni Malipo ya Bima, 3600 ni picha na ufuatiliaji wa Bima);

(v) Kutokana na siku za hivi karibuni kuwepo na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao) ambapo baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo; **kumtaka mzazi husika** atume pesa. ***TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WASHULE KUPATIA NAMBA ZA SIMU ZIFUATAZO;-***

MKUU WA SHULE: **0655 748 374**

MAKAMU MKUU WA SHULE: **0699 460 360**

MTAALUMA **0625 593 389**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**A: NIDHAMU KWA UJUMLA**

1. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuwasalimia walimu/ mtu yeyote mwenye umri mkubwa zaidi yao;
2. Si ruhusa kupiga kelele, kuzungumza au kusababisha usumbufu wowote ndani na nje ya madarasa;
3. Hairuhusiwi kutumia **LUGHA CHAFU** miongoni mwa wanafunzi na kwa mtu mwingine yeyote;
4. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote wa shule;
5. Mwanafunzi anatakiwa kushirikiana na kutenda kazi yoyote atakayoagizwa kuifanya nje ya madarasa pamoja na kushirikiana katika kazi za Elimu ya Kujitegemea;
6. Mwanafunzi haruhusiwi kunywa pombe, kuvuta sigara, kupigana au kuvaa mavazi yenye kuonesha utovu wa nidhamu au kukiuka utamaduni wa Mtanzania;
7. Mwanafunzi anatakiwa kutunza mali zake binafsi na mali za shule ikiwemo vitabu, samani au vifaa vya mabwalo, mabweni, madarasa na ofisi. Pia anatakiwa kutoa taarifa kwa utawala juu ya uharibifu wa mali yoyote ya shule;
8. Kila mwanafunzi anatakiwa awe kwenye msitari wakati wa kupewa huduma yoyote;
9. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa;

10. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kwenda kwenye maeneo yafuatayo bila sababu maalumu au kupewa ruhusa. Maeneo hayo ni Nyumba za walimu na Jikoni;
11. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuingia katika Baa, klabu za usiku na Nyumba za kulala wageni;
12. Awapo shuleni mwanafunzi haruhusiwi kumiliki vitu vya gharama kama redio, kamera simu za mkononi, seti za runinga na vitu vinavyofanana na hivyo. Mwanafunzi akigundulika kumiliki/kutumia vitu hivyo awapo shuleni atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule kabisa;
13. Mwanafunzi haruhusiwi kuleta shuleni vitu vinavyoweza kusababisha ajali ya moto kama mishumaa, viberiti, taa za kandili n.k;
14. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nidhamu nzuri popote pale alipo, ndani na nje ya mazingira ya shule;
15. Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu yeyote ambaye sio mwana jumuiya isipokuwa kwa idhini ya utawala tu;
16. Mwanafunzi akifunga shule au akafukuzwa shule kutokana na tatizo la nidhamu atachukuliwa shuleni na mzazi wake au mlezi aliyethibitishwa na mzazi mwenyewe; na
17. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mawasiliano au kupiga simu kwa mzazi bila ruhusa ya utawala, mawasiliano ya muhimu yatafanyika kwa kuratibiwa na Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule.

**B. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Aina zote za wizi, unyang'anyi, udanganyifu n.k;
2. Ulevi au matumizi ya madawa ya kulevya;
3. Aina zote za makosa ya kujamiana na uasherati. Hii ni pamoja na kukutwa na mikanda ya video, vitabu vichafu vya uasherati au vitu vinavyofanana na hivyo;
4. Kupigana;
5. Makosa ya jinai;
6. Matumizi ya lugha chafu au ya matusi kwa wafanyakazi, wanafunzi wenzake au watu wengineo;
7. Kuolewa au kupata ujauzito;
8. Uharibifu wa mali ya shule au ya wenzake kwa makusudi;
9. Kugoma au kuchochea ghasia;
10. Kuzomea au kuchokoza mwanafunzi au wanafunzi wengine;
11. Kuficha kwa makusudi taarifa ambayo inaweza kusaidia kuzuia kutokea kwa jambo baya au la hatari;
12. Kufanya vitendo vinavyohatarisha maisha yake na wengine kama vile kuumiza wenzake kwa makusudi, kutishia kujiua au kuua wengine;
13. Wizi wa mitihani, kukataa au kutofanya mithani na mazoezi ya masomo bila kutoa sababu za msingi kwa uongozi wa shule;
14. Kuchelewa kuwasili shuleni kutokea likizoni mara tatu mfululizo bila sababu ya maana;
15. Kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa ya utawala;
16. Kulala wawili kitanda kimoja;
17. Kumiliki/kutumia simu na vifaa vinavyoendana na simu ndani ya shule; na
18. Kufanya biashara binafsi au ya mtu mwingine shuleni.

**MUHIMU:**

***Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;***

***Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na***

***mwanafunzi mmoja tu;***

***Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa***).

Fomu zilizoambatishwa zijazwe kikamilifu na zirudishwe shuleni.

i. Fomu rasmi ya kuandikishwa;
ii. Ahadi ya mwanafunzi na mzazi/mlezi;
iii. Fomu ya uchunguzi wa daktari; na
iv. Cheti cha kuzaliwa

**MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA**

**A. KUWAHI**

1. Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni siku aliyoelekezwa;
2. Mwanafunzi anatakiwa kukimbia na kukusanyika uwanjani (assembly ground) pindi asikiapo kengele yoyote ya dharula;
3. Mwanafunzi anapaswa kufika shuleni kabla ya saa 11:00 jioni. Atakayeshindwa kufanya hivyo bila sababu ya msingi, hatapokelewa ndani ya uzio wa shule kwa siku hiyo; na
4. Mzazi au mlezi atawajibika kujaza fomu maalum ya kumchukua (wakati anapomchukua mwanafunzi) na kumrejesha (wakati anapomrejesha).

**B. UVAAJI WA SARE YA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule;

1. Awapo darasani;
2. Awapo nje ya shule au anapohitajika kufanya shughuli rasmi ya shule;
3. Aendapo hospitali;
4. Awapo safarini kwenda au kutoka likizo;
5. Mwanafunzi hatakiwi kuvaa sare ya shule na viatu virefu na/ au mapambo;
6. Mwanafunzi hatarusiwa kuleta shuleni mapambo;
7. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia usafi kama sehemu muhimu ya maisha yake;
8. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa nadhifu awapo kwenye sare ya shule;
9. Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki katika kusafisha mazingira ya shule,

madarasa, mabweni na kadhalika pale anapohitajika kufanya hivyo;

10. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie ukaguzi wa usafi ikiwemo sare za shule, usafi wa mwili, vitanda na guo nyingine;
11. Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha ndefu;
12. Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa nywele mtindo kama kiduku, panki, way n.k;
13. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.

**C. MAHUDHURIO**

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwa darasani kabla walimu hawajaingia; na
2. Ni lazima mwanafunzi kuhudhuria shughuli zote ikiwa ni pamoja na vipindi vyote vilivyoko kwenye ratiba ya masomo, michezo na mikutano ya shule nzima, darasani/mabweni na kazi za nje.

**D. MAANDALIZI YA JIONI NA ASUBUHI**

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwa darasani na kujisomea kwa ajili ya maandalizi ya siku inayofuata kuanzia saa moja na nusu (1:30) jioni hadi saa nne (4:30) usiku. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kupiga kelele au kuwasumbua wenzake wakati wa maandalizi ya asubuhi na jioni; na
2. Mwanafunzi anatakiwa kulala ifikapo saa 5:30 usiku. Taa zote za ndani ya bweni zinatakiwa kuzimwa saa tano na nusu (5:30) usiku isipokuwa za nje, muda huo wanafunzi wote wanatakiwa kuwa vitandani. Mwanafunzi ataamka saa kumi na moja kamili asubuhi na kuhudhuria maandalizi ya asubuhi darasani tangu 11:30 hadi saa moja kamili (1:00) asubuhi.

**E. UTENDAJI KITAALUMA**

1. Kila mwanafunzi ni lazima ajitume katika masomo tangu anaposajiliwa shuleni hadi anapomaliza shule. Mwanafunzi anakiwa kufanya kazi zote anazopewa na walimu, mazoezi na mitihani kulingana na kalenda ya shule na ya Baraza la Mitihani la Tanzania; na
2. Jumamosi ni siku ‘assignment’ ya wiki, hivyo wanafunzi wote wanatakiwa kuwa darasani tangu saa 2:00 asubuhi hadi saa 7:00 mchana.

**F. BWALO**

1. Chakula kitagawiwa kila meza kulingana na idadi ya wana meza husika;
2. Bwalo linatakiwa kuwa safi muda wote na kila mwanafunzi atawajibika kuosha vyombo vyake vya chakula;
3. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia, kuchukua chakula jikoni bila ruhusa au kutupa mabaki ya chakula hovyo;
4. Mwanafunzi atakula chakula kinachopatikana shuleni tu isipokuwa ataruhusiwa kununua vitafunwa vitakavyopatikana hapa shuleni.

**G. MABWENI**

1. Mabweni yote yanatakiwa yawe safi muda wote. Mama mlezi (matron) wa wanafunzi, walimu wa zamu na viranja watafanya ukaguzi wa mabweni. Mashindano ya usafi wa mabweni yatafanyika na bweni litakalopata alama nyingi kwa mwaka mzima litapewa zawadi;

2. Taa zote za chumbani ndani ya mabweni zinatakiwa kuzimwa muda wote wa mchana na baada ya maandalizi ya jioni (5:30 usiku). Hii ni pamoja na kufunga madhubuti mabomba yote ya maji. Feni zote ndani ya chumba zinatakiwa kuwashwa tu wakati wanafunzi wawapo chumbani. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi yeyote kusomea bwenini wakati wa maandalizi ya joini;

3. Hairuhusiwi mwanafunzi kuwa bwenini wakati wa muda wa kuwa darasani au muda wa maandalizi ya asubuhi au jioni, isipokuwa kwa ruhusa maalum kutoka kwa Matron. Wagonjwa wote watapumzika chumba cha kupumzikia wagonjwa (Sick Bay) chini ya uangalizi wa Matron; Ni marufuku kwa wanafunzi kulala wawili katika kitanda kimoja au kulala kwenye bweni/kitanda tofauti na alipopangiwa; na
4. Hairuhusiwi mwanafunzi yeyote kuhifadhi dawa. Dawa zote zitahifadhiwa na Matron na wanafunzi wanaolazimika kutumia dawa watapewa dawa hizo na Matron. Wanafunzi hawataruhusiwa kuingiza kemikali za nywele ndani ya shule. Kemikali hizo zikipatikana zitatupwa na mwanafunzi kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

## H. LUGHA YA MAWASILIANO

Lugha rasmi ya mawasiliano ndani na nje ya madarasa na kwenye shughuli rasmi ni Kiingereza.

## I. HAKI YA KUABUDU

1. Kila mwanafunzi ataruhusiwa kuabudu kwenye dini yake ambayo inafahamika kwa wazazi wake. Kutokana na jiografia ya shule, ibada zote zitafanyika hapa shuleni; na

2. Kila mwanafunzi anapaswa kuvumilia tofauti za wengine za kidini. Shule haitavumilia wenye Imani zilizopindukia (religious extremists) ambao wanaweza kuleta madhara kwao wenyewe au kwa wengine kwa kisingizio cha imani.

## J. WAGENI

1. Wazazi au walezi watawatembelea wanafunzi kwa siku maalum zilizopangwa kama inavyoonyeshwa kwenye kalenda ambayo hupatikana shuleni mwanzoni mwa mwaka wa masomo. Wageni hawaruhusiwi kuingia mabwenini; na

2. Wazazi/ walezi hawaruhusiwi kuwatembelea wanafunzi kinyume na utaratibu huo bila sababu za kimsingi. Hata hivyo wanaweza kufanya miadi na walimu wakati wowote kuzungumzia maendeleo ya mwanafunzi kinidhamu na kitaaluma. Iwapo wazazi watakuja shuleni kwa miadi au kwa dharura nyingine yoyote hawataruhusiwa kuingiza shuleni vyakula au vitu vingine vyovyote visivyoruhusiwa ndani ya shule. Iwapo vitu hivyo vitaingizwa shuleni na kukamatwa, shule haitawajibika kuvirudisha na mwanafunzi atachukuliwa hatua za kinidhamu.

**KIAMBATISHO "A"(TAARIFA ZA MWANAFUNZI)**

**Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi**

| PICHA YA MWANAFUNZI |
|---|
| |

1. Jina kamili la mwanafunzi……………………………………
2. Uraia:………………………………………………………………
3. Dini: ……………………………………………………………….
4. Tarehe ya kuzaliwa:………………………………………….
5. Mahali ulipozaliwa:…………………………………………..
6. Yatima/sio yatima/mzazi mmoja (kata isiyohusika)
7. Shule uliyosoma kabla ya kujiunga na shule hii (jaza jedwali).

| JINA ANDIKISHWA SHULENI | SHULE ULIKOTOKA | MWAKA ULIOANZIA | MWAKA ULIOTOKA |
|---|---|---|---|
| | | | |

Saini ya mwanafunzi: …………………………………………………… Tarehe: …………………………………………………..

**Sehemu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi:**

| PICHA YA MZAZI |
|---|
| |

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi:………………………………………
2. Uraia ……………………………………………………………………
3. Anuani kamili:…………………………………………………………
4. Sehemu unayoishi Wilaya:………………………………………
5. Mtaa:………………………………………… Kata:…………………………………………
6. Namba ya simu………………………. (ya haraka)
7. Jina na mawasiliano ya mlezi wa karibu mjini Dar es Salaam……………………………………

Majina manne ya ndugu wa karibu walioidhinishwa endapo mzazi/mlezi endapo dharura itatokea:

| Na. | Jina | Uhusiano | Anuani na Anakoishi | Namba ya Simu |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

**Maelezo ya kikazi ya Mzazi/Mlezi.**

1. Jina la mwajiri wa Idara……………………………………………………
2. Anuani:……………………………………………………………………
3. Namba ya simu:…………………………………………………………..
4. Kazi ya Mzazi/Mlezi…………………………….(Mfano: Karani,Mwalimu, mkuliuma n.k)

Saini ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………
Tarehe:………………………………….

***NB: Hakikisha unaambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa mwanafunzi.***

**KIAMBATANISHO "B"**
**(HATI YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE)**

Mimi………………………………………………………………………………………………

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote na nimekubali kujiunga na shule hii ya Sekondari
   … ………………………………….. ………………………Kuanzia tarehe……………………………

2. Naahidi kwamba:-

a) Nitazingaitia sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.

b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c) Nitatunza mali ya Umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu darasani na maktaba ya shule na vifaa vya maabara.

d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yoyote stahiki endapo nitakiuka maelekezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

Saini ya mwanafunzi…………………………
……………………………Tarehe………………

**KIAMBATANISHO "C"**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
**This form should be filled by medical Officer**

TO: THE MEDICAL OFFICER

HOSPITAL

……………………………………………………………………………………………………………………
…………………………

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………

Name of student…………………………………………………………………………………….

Age………………. Sex ……………….

Please examine the above named as to her fitness for appointment/re-engagement as a student at

**(To be completed by Medical Officer**)

(A) PHYSICAL EXAMINATION

- Height
……………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………..
- Weight…………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………
- Eye
sight…………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………
- Hearing
……………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………

(B) PAST HISTORY

- Heart
diseases……………………………………………………………………………………………………
……………………………………
- Drug
allergy………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………..
- Asthma……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………….
- Pneumonia………………………………………………………………………………………………
……………………………………………..

(C) LABORATORY TEST

- Stool……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………….
▪Urine……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………….
▪Widal
test……………………………………………………………………………………………………
……………………………………
▪VRDL……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………
▪Blood:
B/S……………………………………………………………………………………………………
…………………………………
▪Blood
Group…………………………………………………………………………………………….......
…………………………….
▪Hb……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………….
▪Tuberculosis…………………………………………………………………………………………
▪HIV……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

I have examined the above named and consider that she is physically fit/unfit for appointment /
re-engagement are as above.
Name of Authorized
Doctor…………………………………………………………………………….
Signature……………………………………………………………………………………………

Designation…………………………………………………………………………

Date and official
Stamp…………………………………………………………………………………………………